



# SAYANSI YA UPENDO

SAYANSI INADHIBITISHA YA KWAMBA UPENDO, USIKIVU NA UCHANGAMFU WA WAZAZI NI VITENDO VYA MUHIMU KWA UKUAJI WA WATOTO WAO. FAIDA YA VITENDO VINA-VYOONYESHA UPENDO HUDUMU KUTOKA UTOTONI HADI UTU UZIMA.



KADIRI MTOTO ANAVYOPATA UPENDO, NDIVYO IMANI NA HAMU YAKE YA KUCHUNGUZA ULIMWENGU INAKUA.

MGUSO WA MWANADAMU NI MUHIMU KWA UKUAJI WA UBONGO NA UKUAJI WA MWILI.

KUONYESHA KUJALI KUPITIA VITENDO KAMA VILE KUKUMBATIA, KUSHIKANA MKONO NA KUMPIGAPIGA MTU BEGA KWA UPENDO HUNUFAISHA WOTE, MTU ANAYETENDA HIVI VITENDO NA ANAYETENDEWA.

OXYTOCIN (KEMIKALI ILIYO MWILINI) HUCHOHEA UKUAJI, KUIMARISHA MFUMO WA KINGA NA HATA KUSAIDIA MAJERHA KUPONA HARAKA.

PIA, HUPUNGUZA MSONGO WA MAWAZO, HUONDOA WASIWASI WA KUPITILIZA, NA HATA KUPUNGUZA SHINIKIZO LA DAMU.

HII INAWAFANYA WATOTO WAKUE KUWA WATU NADHIFU, WENYE AFYA NJEMA NA WASTAHIMILIVU.

UPENDO KWA NJIA YA VITENDO HUJENGA UAMINIFU NA KUFANYA KAZI KAMA DARAJA LINALOSAIDIA WAZAZI NA WATOTO WAO KUWA NA UHUSIANO MZURI.

UPENDO HUWAFANYA WATOTO KUHISI KUWA WANAPENDWA, HUJENGA USTAHIMILIVU WAO NA HUWAFANYA KUWA NA NGUVU ZAIDI.

